***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.... Kazi iendelee!***
***Mahakama ya Tanzania..... uadilifu, weledi na uwajibikaji!***

Kwanza, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kukutana hapa kwa ajili ya Jubilei ya miaka 25 ya Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake Tanzania (TAWJA). Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa heshima aliyonipa ya kumwakilisha kama Mgeni Rasmi kwenye ufunguzi wa Jubilei ya Miaka 25 ya TAWJA.

Aidha, kwa kutumia fursa hii nampongeza Mwenyekiti wa TAWJA Mheshimiwa Jaji Barke Sehel, viongozi wenzake na wenyeviti wa TAWJA waliopita, kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kipindi chote cha miaka 25 ya TAWJA. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Jaji Eusebia Munuo, Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufaa pamoja na waanzilishi wengine wa TAWJA kwa maono yaliyopelekea kuanzishwa kwa Chama hiki hapa nchini. Nafahamu TAWJA imepiga hatua kubwa tangu kuanzishwa kwake na tayari tumeelezwa baadhi ya mafanikio yaliyofikiwa yakiwemo: kuchangia marekebisho ya sheria, hususan Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kwa kuongeza kifungu kinachohusu rushwa ya ngono ili kudhibiti matumizi mabaya ya madaraka yanayohusisha rushwa ya ngono; kuandaa mwongozo wa majaji na mahakimu katika kushughulikia kesi za ukatili wa kijinsia Tanzania Bara; kushiriki maadhimisho ya siku ya majaji duniani na kubadilishana uzoefu na majaji wa nchi nyingine kwa lengo la kuongeza kasi ya kutafuta haki na usawa wa kijinsia; kulea na kukuza vipaji vya wanachama wake; na kuendelea kutoa elimu kuhusu haki na usawa miongoni mwa jamii ya watanzania. Kwa ajili hiyo, napenda kuipongeza TAWJA kwa mafanikio hayo katika utekelezaji wa malengo yake katika kipindi hiki cha miaka 25. ***Hongereni Sana!***

***Mheshimiwa Jaji Mkuu,***
Kaulimbiu ya maadhimisho ya Jubilei ya miaka 25 ya TAWJA inayosema **"Jubilei ya Miaka 25 ya TAWJA: Kusherehekea Utofauti na Mshikamano katika Usawa wa Kijinsia"**, ni muafaka kwa kuwa inatukumbusha kazi ambayo TAWJA imekuwa ikifanya katika kuleta usawa na kupinga ukatili wa kijinsia. Pia, inatuhimiza kutambua kuwa tofauti za kijinsia zilizopo siyo msingi wa kubaguana, badala yake tunapaswa kutumia tofauti hizo kujenga mshikamano na usawa wa kijinsia. Kama tunavyofahamu, haki na usawa ni msingi ambao unajenga jamii inayothamini utu wa kila binadamu, bila kujali jinsia, rangi, kipato, elimu au asili. Hivyo, katika muktadha wa usawa wa kijinsia, mshikamano unamaanisha umoja utakaohakikisha kuwa fursa na haki zinapatikana kwa wote na kwa usawa. Hivyo, napenda kutoa wito kwa watanzania wote, taasisi za kitaifa na kimataifa na mashirika yasiyo ya kiserikali kushiriki katika kupigania haki na usawa wa kijinsia hapa nchini na duniani kote.

***Mheshimiwa Jaji Mkuu,***
Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imejizatiti kuimarisha usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake hapa nchini kwa kuanzisha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambayo inasimamia masuala ya usawa wa kijinsia.

Dhamira hiyo ya Serikali inaonekana zaidi kupitia mikakati, mipango na sera za kitaifa kama vile Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano (2011/12–2015/16, 2016/17 – 2020/21 na 2021/22 – 2025/26), Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (NSGR) na Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya 2000. Aidha, Serikali ya Tanzania imesaini na kuridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa inayotambua na kulinda usawa wa kijinsia. Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imedhihirisha kwa vitendo dhamira yake ya kuboresha utendaji katika utoaji haki, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha usawa wa kijinsia katika ngazi mbalimbali za uongozi wa Mahakama. Mathalan, kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Jaji Mkuu, mfumo wetu wa Mahakama umefikia mafanikio makubwa katika kukuza usawa wa kijinsia. Katika Mahakama ya Rufani, 33% ya Majaji ni wanawake; Mahakama Kuu, ni 38%. Uwiano huu umejidhihirisha pia kwa Wasajili ambapo wanawake ni 33% na Naibu wasajili, 48.72%. Aidha, wanawake ni 50% ya Mahakimu wa Mahakama za Mahakimu Wakazi na 41% ya Mahakimu wa Mahakama za mwanzo. Takwimu hizi zinadhihirisha dhamira ya dhati ya kufikia usawa katika utendaji wa Mahakama ya Tanzania, katika masuala ya ajira na nafasi za maamuzi.

***Mheshimiwa Jaji Mkuu,***

Pamoja na dhamira njema ya Serikali ya kuhakikisha usawa wa kijinsia hapa nchini, bado wanawake ambao idadi yao ni zaidi ya nusu ya watu hapa nchini, wanapewa nafasi ndogo  katika umiliki wa mali na wanabaguliwa kwa msingi wa jinsia. Kwa mujibu wa Mpango wa Kitaifa wa Kupinga vitendo vya Kikatili dhidi ya Wanawake wa mwaka 2016, kati ya wanawake kumi, 4 wamepitia ukatili wa kimwili, na mmoja kati ya watano wamepitia ukatili wa kingono maishani mwao wakiwa na umri mdogo (chini ya miaka 15). Kulingana na Ripoti ya *UN Women Social Institution and Gender Index* (SIGI) 2022, ukatili wa kijinsia nchini Tanzania unabainishwa zaidi kupitia ndoa za utotoni, ubaguzi ndani ya familia, ukatili dhidi ya wanawake, ukosefu wa uhuru katika kupanga uzazi, upatikanaji na umiliki wa ardhi. Aidha, kulingana na Taarifa ya Tathmini ya Ukatili wa Kijinsia Tanzania iliyoandaliwa na Benki ya Dunia mwaka 2022, 40% ya wanawake wote wenye umri wa miaka 15 hadi 49 wamefanyiwa ukatili wa kimwili na 17% wamepitia ukatili wa kingono. Aidha, taarifa hiyo inaeleza zaidi kuwa 44% ya wanawake wenye umri wa miaka 15-49 wamepitia ukatili wa kingono au kimwili na wenza wao na ndugu wa karibu. Kwa mujibu wa tathmini hiyo, takriban 30% ya wasichana wamepitia ukatili wa kingono kabla ya kufikia umri wa miaka 18. Imeelezwa zaidi kuwa, wastani wa kuenea kwa ukeketaji kwa wanawake na wasichana kote nchini ni 10%. Vilevile, Taarifa hiyo inaeleza kuhusu jinsi jamii inavyohalalisha unyanyasaji, ambapo 58% ya wanawake na 40% ya wanaume wanaamini kuwa mume anayo haki ya kumpiga mke wake katika mazingira fulani.

***Mheshimiwa Jaji Mkuu,***

Katika kusheherekea Utofauti na Mshikamano katika Usawa wa Kijinsia, jamii yetu haina budi kuendelea kuchukua hatua madhubuti katika kukabiliana na vitendo vya

ukatili wa kijinsia hapa nchini. Kwa msingi huo, napenda kutumia fursa hii kutilia mkazo mambo yafuatayo:

**Kwanza;** napenda kutoa wito kwa Majaji na Mahakimu wanawake nchini walioko katika utumishi na waliostaafu, kuhakikisha wanajiunga au wanahuisha uanachama wao wa TAWJA kwa kulipa ada. TAWJA inahitaji mshikamano na ushiriki wa wanachama wake wote ili kufikia malengo yake. Ninafahamu kuhusu changamoto ya ufinyu wa muda kwa wanachama walioko kwenye utumishi, hivyo ninashauri kuendelea kutumia uzoefu wa wanachama waliostaafu katika kutekeleza baadhi ya majukumu ya TAWJA. Idadi ya Majaji na Mahakimu wanawake waliokuwepo miaka 25 iliyopita ni ndogo ikilinganishwa na sasa, hivyo endapo wote watakuwa wanachama hai, TAWJA itaweza kupiga hatua kubwa katika kufikia malengo yake.

**Pili;** ni kuhusu kufumbia macho vitendo vya ukatili. Wapo wanawake, watoto na wanaume wanaopitia vitendo vya ukatili wa kijinsia au kimwili lakini hawatoi taarifa kwenye vyombo vya sheria ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. Aidha, baadhi ya mila na desturi katika jamii zimekuwa zikitumika  kuwakandamiza waathirika. Hali hii ya waathirika wa vitendo vya ukatili kutokutoa taarifa kwenye mamlaka husika inachangia kushamiri kwa vitendo hivi. Natoa wito kwa Watanzania wote kuibua taarifa kuhusu vitendo vya ukatili ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa dhidi ya wahusika.

**Tatu,** ni kujenga tabia ya kutambua na kusheherekea mafanikio ya wanawake katika jamii ili kutoa hamasa kwa wasichana na wanawake wengine kujifunza na kuiga mifano hiyo. Tunayo mifano ya wanawake hapa nchini waliofanya vizuri katika fani mbalimbali tukianza na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa kwanza mwanamke; Bibi Titi Mohamed, mwanamke aliyekuwa mstari wa mbele katika kupigania uhuru wa nchi yetu; Mhe. Julie Manning mwanamke wa kwanza Mtanzania kusoma sheria na baadaye kuwa Jaji wa Mahakama Kuu; Mhe. Jaji Eusebia Munuo, Jaji wa kwanza mwanamke Mtanzania wa Mahakama ya Rufani; Mhe. Anne Makinda, Spika mwanamke wa kwanza wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Meja Jenerali Zawadi Madawili, mwanamke wa kwanza kushika Cheo cha Juu Jeshini; Prof. Verdiana Masanja, mwanamke wa kwanza kutunukiwa shahada ya uzamivu katika Hisabati na Profesa wa Hisabati mwanamke wa kwanza nchini; Prof. Esther Mwaikambo, daktari wa kwanza mwananmke, na wengine wengi. Katika hili, naitaka TAWJA kutafsiri kwa vitendo programu ya Wanawake katika Uongozi wa Sheria (Women in Leadership in Law – WILIL) ili kuandaa viongozi wengi wanawake watakaoshika nafasi mbalimbali za uongozi nchini.

**Nne,** ni elimu kwa jamii kuhusu TAWJA na malengo yake na kuhusu masuala ya haki na usawa wa kijinsia kwa kutumia njia mbalimbali kama vile mitandao ya kijamii, televisheni, redio, na muziki. Aidha, napenda kutoa wito kwa wazazi na walezi kuhakikisha wanatoa fursa sawa ya elimu kwa watoto wote. Vilevile, kwa kuzingatia mazingira ya sasa, kumeanza kuwa na matukio mengi ya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto wa kiume. Kwa ajili hiyo, tunapopigania haki na usawa wa mtoto wa kike, napenda kusisitiza kuwa mtoto wa kiume asiachwe nyuma.

Mwisho, napenda kumalizia hotuba yangu kwa kuupongeza kwa dhati Mhimili wa Mahakama kwa kuendelea kusimamia utoaji haki nchini na kuchangia katika kuimarika kwa uchumi wa Taifa na upatikanaji wa huduma muhimu za jamii. Aidha, naipongeza TAWJA kwa kutimiza miaka 25 ya utetezi wa haki za wanawake, watoto na wenye mahitaji maalum, pamoja na kutetea haki za binadamu kwa ujumla pasipo kujali rangi, jinsia, hadhi au dini. Kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninayo heshima sasa kutamka kuwa Jubilei ya miaka 25 ya Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake Tanzania (TAWJA) imefunguliwa rasmi. Nawatakia maadhimisho mema!

**Asanteni sana**